International Journal of Advanced Education and Research
ISSN: 2455-5746, Impact Factor: RJIF 5.34
www.alleducationjournal.com
Volume 1; Issue 9; September 2016; Page No. 19-27

# Ufafanuzi wa vichocheo vya migogoro ya kindoa kama vinavyosawiriwa katika riwaya ya *kidagaa kimemwozea* na ken walibora, Kenya

[1] Nyamete Florence, [2] Francis Aswani Buliba, [3] Dr. Nicholas Goro Kamau

[1] Laikipia University, Kenya
[2] Prof. Laikipia University, Kenya
[3] Laikipia University, Kenya

**Ikisiri**

Kumekuwa na ongezeko la migogoro ya kindoa katika jamii mbalimbali. Kumekuwa na ugomvi, vita, talaka na hata mauaji katika ndoa mbalimbali. Chanzo cha migogoro hii si dhahiri ingawa baadhi ya kazi za sanaa zimeangazia taasisi ya ndoa. Utafiti huu uliazimia kuchunguza usawiri wa migogoro ya kindoa katika riwaya teule kutoka Afrika mashariki. Kutokana na utafiti huo, makala hii inaashiria kufafanua vichocheo vya migogoro ya ndoa kama vinavyosawiriwa katiak riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na Ken Walibora. Migogoro ya kindoa ni mojawapo ya mambo ibuka ambayo hayajatafitiwa kwa kina na waandishi wengi. Utafiti huo uliazimia kujaza pengo hili kwa kuchunguza usawiri wa ndoa katika vitabu teule. Riwaya hii inaipa asasi ya ndoa umuhimu sana. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhalisia. Nadharia hii hueleza kwamba fasihi ni uwakilishi wa matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi. Utafiti huo umehusisha uchunguzi wa maudhui ya migogoro ya kindoa kupitia kwa usawiri wa wahusika katika riwaya teule. Utafiti huo ulikuwa ni wa maktabani. Riwaya teule na kazi zozote ambazo zinahusiana na mada ya utafiti zilisomwa. Sampuli ilichaguliwa kwa mbinu ya kimakusudi. Data ya kimsingi ilitoka kwenye riwaya tatu teule: *Utengano, Kidagaa Kimemwozea* na *Mwisho wa Kosa.* Data imekusanywa kuzingatia migogoro iliyoelezwa katika riwaya hizi teule, athari zao na kupambanua njia zinazodhihirika za kukabiliana na migogoro hiyo. Utafiti huu ni wa kimaelezo na data imechanganuliwa kwa njia ya kiuthamano. Matokeo ya kazi hii yamedhihirisha kwamba kuna vichocheo vya migogoro ya kindoa ambayo husababisha athari mbalimbali kwa familia na jamii. Inatarajiwa kwamba matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa kwa wasomi wa fasihi kuhusiana na dhima ya fasihi katika jamii.

**Maneno Muhimu:** Vichocheo, Migogoro, Kindoa, Riwaya, *Kidagaa Kimemwozea*

## Utangulizi

Ndoa, kulingana na Maitaria (2012, uk. 10) [15], ni makubaliano kati ya mwanamume na mwanamke kuwa na uhusiano wa kudumu kama mume na mke. Uhusiano huu unaweza kuwashirikisha watu wa ukoo katika uteuzi wa mchumba au wanaotaka kuoa na kuolewa kuchaguana wao wenyewe. Ndoa ni ukamilifu wa makubaliano ya muungano wa mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kuwa ni mume na mke kulingana na sheria, mila, au desturi za sehemu fulani

Kulingana na Collins na Anderson (2006) [6], ndoa ni hali au uhusiano wa kuwa mke na mume. Wanasema pia inaweza kufasiliwa kama muungano wa kisheria au maagano yaliyofanywa baina ya mwanaume na mwanamke kuishi pamoja kama mume na mke. Katiba ya Kenya (2010, uk. 33) [25] katika ibara ya 45 inasema kuwa familia ndicho kiungo cha kimsingi cha jamii na muhimu katika kuleta utaratibu wa kijamii. Pia inasema kuwa kila mtu mzima ana haki ya kumwoa mtu wa jinsia nyingine, lakini lazima pawe na makubaliano baina yao wawili. Ndoa ni asasi muhimu ya kijamii kwani kupitia kwayo jamii inaendeleza kizazi.

## Mapitio ya Maandishi Kuhusu Mada Ya Utafiti

Waandishi mbalimbali wamezungumzia suala la ndoa na migogoro ya kindoa katika jamii. Maitaria (2012, uk. 22) [15] anasema kuwa ndoa ni asasi muhimu katika jamii. Kuna ndoa ambazo wazazi, walezi au watu wa ukoo huwachagulia wana wao wachumba na zile ambazo vijana wenyewe hujichagulia. Ndoa ambazo huzingatia uteuzi wa wazazi huwa ni zile zilizojikita katika utamaduni wa jamii. Iwapo mwana atajichagulia yeye mwenyewe, huchukuliwa kuwa amevunja miiko ya utamaduni. Maitaria (2012) [15] anaendelea kusema kuwa kwa sababu ya ndoa kuingiliwa na mawazo ya kitamaduni kunakuwa na mgogoro kati ya mume na mke katika ndoa.

Wataalam kadhaa wa nadharia ya ufeministi, wakiwemo Bouchier (1983) [3], Engels (1985) [9], Ramazonoghlu (1989) [21], Rao (1983) [22], Cutrufelli (1987) na Eagleton (1989) [8], wanapinga dhuluma zinazowakumba wanawake kwa sababu ya jinsia yao. Wataalam hawa wanakubaliana kuwa nadharia ya Ufeministi (Uake) hulenga kuyafichua madhila yanayowapata wanawake katika jamii na kunawasua kutoka kwa madhila hayo.

Greer (1970) [11] ameisawiri ndoa kama asasi sumbufu kwa mwanamke. Anawahimiza wanawake kususia ndoa kwa kuwa hali ya kuolewa inawafanya kumilikiwa na wanaume wao na hivyo wapoteze uhuru wa utambulisho wao na uhuru wao. Katika utafiti wetu tumechunguza migogoro inayoikabili ndoa, athari zake na njia za kukabiliana na migogoro hiyo. Vilevile, Maina (2005, uk. 38-40) [14] anasema kuwa hali ya mwanamke kulipiwa mahari anapoolewa humfanya achukuliwe kama mali ya mumewe na hili ni tatizo kubwa. Utafiti huu umetusaidia kuangazia visababishi vya migogoro ya kindoa.

Wamitila (2002, uk. 157-158) [28] anaeleza kuwa ndoa kama asasi ya kitamaduni inaendeleza ukandamizaji wa wanawake.

Imejengwa kwenye msingi wa itikadi ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume, naye mwanamke akawa anachukuliwa kama chombo tu. Utafiti wetu umechanganua mchango wa mume na mke katika migogoro ya kindoa. Katola (2006, uk. 75-81) [12] akichunguza udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili, anasema kuwa baadhi ya taasisi kama ndoa zinatumiwa kumdhulumu mwanamke na zafaa kubadilishwa au kuondolewa. Utafiti wetu umeangazia visababishi vya dhuluma dhidi ya wanandoa wa jinsia yote mbili.

Nyaosi (2008) [19] ametafitia taswira ya ndoa katika riwaya za Kiswahili, *Kiu* (1972) na *Msimu wa Vipepeo* (2006). Aligundua kuwa asasi ya ndoa ina matatizo mengi yanayomkumba mwanamke na hadhi yake katika ndoa, ni ya chini. Yaani,mwanmke ni mshirika nambari ya pili katika ndoa. Ndoa imesawiriwa kama nyenzo inayotumiwa kumdhalilisha mwanamke. Mchango wake umekuwa wa maana katika utafiti wetu kwa kuangazia visababishi vya dhuluma na unyanyasaji katika ndoa.

Kuhusu mgogoro wa kindoa, Arege (2012, uk. 5-6) [2] anaeleza kuwa mgogoro wa kindoa unaweza kusababishwa na mgongano wa desturi na mitazamo tofauti kati ya mume na mke. Arege (2012, uk. 62-63) [2] anaendelea kusema kuwa waliooana lazima wawajibike katika kuikimu familia yao hasa mwanamume lazima awe na uwezo wa kuikimu familia yake la sivyo kunatokea mgogoro. Arege (2012) [2] anaeleza kuwa watu katika ndoa hupitia matatizo mbalimbali na wasipovumiliana ndoa haiwezi kudumu. Ndoa nyingi hazifungwi kwa sababu ya mapenzi bali kwa sababu ya utajiri wa mtu. Ndoa kama hizi ambazo hazizingatii mahusiano mema baina ya wanaooana hazidumu. Arege anabeza ndoa ambazo watu wanaweka mali mbele badala ya mapenzi. Maelezo haya ni muhimu katika makala hii yetu kwa kubainisha vichocheo na athari za migogoro ya kindoa.

**Suala la Utafiti**

Kumekuwa na ongezeko la migogoro ya kindoa katika jamii mbalimbali. Kumekuwa na ugomvi, vita, talaka na hata mauaji katika ndoa mbalimbali. Chanzo cha migogoro hii si dhahiri ingawa baadhi ya kazi za sanaa zimeangazia taasisi ya ndoa. Utafiti huu uliazimia kuchunguza usawiri wa migogoro ya kindoa katika riwaya teule za Kiswahili: *Utengano* (1980) na Said Ahmed Mohamed, *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na Ken Walibora na *Mwisho wa Kosa* (1987) na Burhani Zainabu. Katika utafiti huo tulichanganua migogoro ya kindoa, athari za migogoro hiyo kwa jamii na tumepambanua njia zinazodhihirika za kukabiliana na migogoro ya kindoa katika riwaya teule. Kufuatana na utafiti huo, makala hii inaangazia jambo la migogoro ya kindoa ya kindoa kama ilivyoswiriwa na Ken Walibora katika riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea.*

**Nyenzo Na Njia**

Utafiti huu ni wa kimaelezo. Vilevile, utafiti ulikuwa ni wa kifasihi na ulifanyika maktabani. Tulisoma kazi mbalimbali zinazoangazia suala la utafiti na tumeeleza mitazamo yao kuhusu migogoro ya kindoa. Pia tumeelezea nadharia ya Uhalisia na vile nguzo zake zilitumika kuongoza utafiti huu. Riwaya tatu teule za Kiswahili, *Utengano*, *Kidagaa Kimemwozea* na *Mwisho wa Kosa*, zililengwa kwa sababu zinaipa asasi ya ndoa umuhimu sana. Tulisoma riwaya hizi kwa kuzingatia vipegele vya wahusika, mandhari, mbinu za sanaa zinazotuelekeza katika maudhui ya asasi ya ndoa na migogoro ya kindoa. Tumechambua mahusiano ya wahusika walio katika ndoa, walio na mahusiano ya kimapenzi na waliotalikiana na athari ya mahusiano hayo kwa familia na jamii.

Utafiti huu ulizingatia sampuli ya kimakusudi. Usampulishaji wa aina hii huhusisha uteuzi wa sehemu fulani kama eneo la utafiti, kazi teule au watu fulani kama wasailiwa. Kazi hizo au sehemu hiyo huteuliwa kwa kuzingatia sababu maalum (Mugenda & Mugenda, 1999) [16]. Riwaya hizi ziliteuliwa kwa kutumia sampuli makusudi. Data ilipatikana kwa kusoma riwaya teule na kuchambua maudhui ya migogoro ya kindoa kwa kutumia vipengele vya wahusika, mbinu za sanaa, mandhari na kubainisha vichocheo vya migogoro ya kindoa, athari za migogoro hiyo kwa jamii na kupambanua njia zinazodhihirika katika riwaya hizi za utafiti za kukabiliana na migogoro ya kindoa.

Data iliyotumika katika utafiti huu ilitokana na upekuzi wa riwaya tatu za utafiti; *Utengano, Kidagaa Kimemwozea* na *Mwisho wa Kosa*. Vile vile tulisoma makala ya maandishi ya wataalamu wengine yaliyo na uhusiano na mada yetu ya utafiti. Tulisoma riwaya za utafiti na kufafanua vichocheo vya migogoro ya kindoa kama vinavyosawiriwa katika vitabu hivi kwa kuangalia uhusiano miongoni mwa wanandoa, walio na uhusiano wa kimapenzi na waliotalikiana.

**Matokeo Na Majadiliano**

Migogoro ni kitu cha kawaida katika uhusiano wa ndoa na kwa hakika haiepukwi. Kuna vichocheo vingi ambavyo vinaweza kusababisha migogoro katika mahusiano au ndoa na vinatofautiana kutoka uhusiano mmoja hadi mwingine. Hapa tumeeleza visababishi vikuu ambavyo kwa kawaida hutokea karibu kila mahusiano ya ndoa.

**Wivu Uliokithiri na Mashaka**

Wivu na mashaka vinatokana na jinsi ambavyo mpenzi mmoja anavyohusiana na watu wengine wa jinsia tofauti. Inaweza ikawa marafiki, wafanyikazi wenza au wapenzi wa zamani. Pia unaweza kutokana na mwingine kumshinda mwingine katika hali fulani kama cheo na mshahara. Vyovyote vile, itakavyokuwa ni kwamba wivu unasababisha ugomvi katika mahusiano mengi. Mke au mume, kwa kutokujiamini kwake, anaweza kujikuta anaanza kuhisi kutishiwa nafasi yake na kitu au mtu mwingine. Wachunguzi wa mahusiano wanasema kuwa wivu hauwezi kwenda pamoja na mapenzi. Wivu wa kupindukia unaweza kusababisha ugomvi ambao nao ni sababu kubwa ya kuachana kwa wapenzi. Wivu husababishwa zaidi na kutokujiamini kwa mtu.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* Mtemi Nasaba Bora anamshuku bibiye Zuhura kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kijana mfanyikazi wao, Amani. Huu ni wakati alimpata Amani katika chumba chao cha kulala. Amani alikuwa ameitwa na Zuhura chumbani kuwa alikuwa ameona kitu. Kilikuwa ni kitu kama panya. Huku wakiendelea kuangazaangaza mvunguni, Mtemi akawakuta. Akawashuku kuwa walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Alimpiga sana Amani hadi akadhani amekufa na kwenda kumtupa kando ya Mto Kiberenge. Mgogoro ukashuka na Bi. Zuhura akapewa talaka. Mwandishi anaeleza,

Mtemi Nasaba Bora alisimama jadidi na kuwatazama hawa watu wawili waliosimama wima kutetemeka kama waliokuwa wamepigwa na dholuba ya theluji. Alikuwa ameyakinisha tuhuma yake ya siku nyingi. Kumbe huyu mwanamke hunienda kinyume na mfanyakazi jamani? (uk. 131).

Mtemi Nasaba Bora aliamini kuwa mkewe alikuwa anazini na Amani.

**Tendo la Ndoa**

Greer (1970:30) [11] anadai kwamba wanawake kwa kiasi wametenganishwa na ashiki yao ya kimapenzi na jamii imefanya tendo la ndoa kuwa ni himaya ya wanaume na kazi ya wanawake ni kuwaridhisha wanaume tu kimapenzi huku wakiachwa wakiumia kihisia. Hali hii ndiyo inayosababisha migogoro miongoni mwa wanandoa.

Ijapokuwa suala la kufanya mapenzi si kila kitu kwa wapenzi ndani ya nyumba, lakini linachangia sana katika kuleta ugomvi aina yao. Kufanya mapenzi kupita kiasi au mara chache kunaleta matatizo kwa wapenzi hasa ambao wana uhitaji tofauti. Tendo la ndoa ni muhimu kwa wanandoa kwa vile linahusiana na hisia za kimwili. Inawezekana ikawa kiwango cha mapenzi, ladha ya mapenzi au ufundi, umepungua au umeisha kabisa. Wakati mwingine ni mapenzi ya mgao kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuwa na shughuli nyingi za kikazi au kwa sababu ya matumizi ya madawa ya kulevya na ulevi wa kupindukia. Sababu nyingine ni pengine mwanandoa mmoja ana mtu mwingine pembeni au amechoshwa na mapenzi ya aina moja kila siku. Jambo hili linajenga kutojiamini, upweke na kupoteza uaminifu.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, kuna mgogoro kati ya Mtemi Nasaba Bora na mkewe Bi. Zuhura. Ndoa baina ya Bi. Zuhura na Mtemi Nasaba Bora ilikuwa imejaa mateso, unyanyasaji na kutoaminiana. Bi. Zuhura alikuwa mpweke. Haja zake kutoka kwa mume wake hazikutimizwa. Mtemi Nasaba Bora alikuwa anaamka akiwa amechelewa mara nyingi kwa sababu alifika nyumbani na kulala akiwa amechelewa. Hii ni kwa sababu alikuwa mwenye shughuli nyingi alizoziita shughuli za kutatua 'mgogoro wa ardhi' (uk. 90). Bi. Zuhura alikuwa amemzoea mumewe kuchelewa siku nyingi. Hata Bi. Zuhura alikuwa anasononeka kwa kuachiwa upweke wa mapenzi wakati wote huu. Mwandishi anasema,

Bi. Zuhura alipojilaza katika kitanda chao chenye matendegu ya msonobari na godoro lenye maki pana, alitafunwa na ukiwa na jakamoyo. Mume ajaye usiku wa manane au jogoo la kwanza na kujibwaga kitandani kama gogo la mti ni mume gani? … Aliwaonea gere wanawake wengine ambao walishinda pamoja na wanaume zao na kukesha nao na kugandiana kwa mapenzi yasiyojua kufa. Alijiona maskini wa mapenzi katikati ya mali isiyokadirika (uk. 90).

**Kukosekana kwa Uaminifu katika Ndoa**

Uaminifu ni suala muhimu sana katika ndoa. Wanandoa kutokuwa waaminifu hutia doa katika ndoa yao. Chapman (2008, uk. 169-170) [5] anasema kuwa sifa ya kupendelea uaminifu katika ndoa imejikita katika ubinadamu wetu, na inahusika na uadilifu na unyoofu. Kulingana na sheria za Kenya juu ya Masuala ya Ndoa (1962, uk. 7), panapo ushahidi dhahiri kuwa mwanandoa si mwaminifu, mwenzake anaweza kumtaliki au adai kutalikiwa. Kutoaminiana katika ndoa huzaa tuhuma, uongo, na hata ugomvi.

Kushindwa kutimiza ahadi, kusema uongo au kufanya usaliti wa kimapenzi ni mambo ambayo humwondolea mtu uaminifu kwa mwenzake. Kukosekana kwa uaminifu ni sababu kuu ya kusababisha mgogoro na kuyumba kwa mahusiano au ndoa. Iwapo kuaminiana kwa msingi kabisa katika uhusiano kutavunjwa mara kwa mara, hasira za mpenzi kwa mwenzake zitalimbikizwa na hamu ya wenza kuendelea kuishi pamoja itapungua. Hakuna kitu kibaya kama uongo na usiri. Uongo wa aina yoyote ile si mzuri katika ndoa kwa sababu huweza kupunguza mapenzi na uaminifu kwa kiasi kikubwa sana miongoni mwa wanandoa.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* ndoa ya Mtemi Nasaba Bora na Zuhura imekumbwa na ukosefu wa uaminifu. Mtemi Nasaba Bora mara kwa mara alidanganya kuwa anakwenda kusuluhisha 'migogoro ya mashamba' kumbe alikuwa anatembea na wanawake wengine kama Lowela binti Maozi. Alimpa Lowela ujauzito na kuzaa naye kitoto Uhuru. Fauka ya haya, alimpeleka shambani kwake Baraka ambako alikuwa akienda kumtembelea. Bibiye Zuhura alimtuhumu lakini hakuweza kumuuliza mumewe kilichokuwa kinaendelea (uk. 39).

Bi. Zuhura alikihurumia kitoto hicho… Kilifanana na mtu fulani pale kwenye kasri la Majununi. Bi. Zuhura alishindwa kutambua kama mshabaha huo ulikuwa sadfa tupu au palikuwa na uwezekano wa … Haidhuru …watu wote walitoka kwa Adamu na Hawa (uk. 39).

**Matarajio**

Kuna baadhi ya watu wanaoingia katika ndoa wakiwa na matarajio mengi na hali hii inakuwa tofauti wakishaingia ndani ya ndoa. Matarajio ya watu wengi wanapoingia katika ndoa huwa ni kupata faraja, kuondoa upweke na kupata rafiki. Wapo wengine wanaoingia kwenye mahusiano kwa sababu zisizo za kimapenzi. Hapa kuna mambo kama mali, fursa, sifa za marafiki na mashinikizo mengine ikiwamo kupata ujauzito. Wengine wanaingia kwenye mahusiano wakiwa na taarifa zisizo sahihi kuhusu ndoa na kukatishwa tamaa na uhalisia wa mambo unapoingia kwenye mahusiano na hatimaye mambo kuweza kwenda mrama. Wachache wa wanaoingia katika ndoa hufikiria kukutana na vikwazo vya kimaisha. Tafiti zinaonyesha kuwa wakati mtu anapotafuta mpenzi huamini kutoka moyoni mwake kuwa akiwa na mwenzake, matatizo ya upweke, kukosa msaada wa hili na lile yatakwisha lakini baadaye anakuja kubaini kuwa aliyokusudia kuyapata hayapati tena na hivyo kujuta.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* Majununi alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na msichana Mfaransa. Msichana huyo alikuwa na matarajio ya kuishi katika maisha ya hali ya juu. Majununi alijenga nyumba na akaiita kibanda. Alitarajia Majununi kumjengea jumba kubwa kulingana na daraja lao. Hata hivyo, Michelle na Majununi hawakuelewana kuhusu jumba alilojenga Majununi. Michelle alimwambia Majununi, "Niwie radhi sana lakini naona hatufaani. Katafute mwanamke kufu yako" (uk. 18).

Dora alipoolewa na Mwalimu Majisifu alitarajia kuwa na maisha mazuri, ya furaha na kusaidiana kwa kila hali. "Dora alisimama sebuleni na kumwangalia mumewe aliyekuwa kajinyosha kochini kalewa chopi. Haya ni maisha gani? Alikeketeka maini Dora. Alijutia siku aliyokubali kufunga pingu za maisha na Mwalimu Majisifu" (uk. 44). Bi. Zuhura alitarajia ndoa yao kuwa ya furaha lakini ikawa sivyo. Aliishi maisha ya upweke na uoga. Mumewe Mtemi Nasaba Bora hakuwa na wakati wa kukaa naye na hata kumtimizia haja zake za kimapenzi. Bi. Zuhura aliishi maisha ya kuvumilia na kujuta. Aliwaonea gere wanawake wengine ambao walishinda pamoja na wanaume zao na kukesha nao na kugandiana kwa mapenzi yasiyojua kufa.

## Ubinafsi na Kiburi

Arege (2006) [1] anafafanua ubinafsi kuwa ni hali ya mtu kufanya mambo au kuchukua hatua ambazo zinalenga kuyakidhi masilahi yake tu. Huwa hajali maslahi ya wengine. Sayers (1987) [26] amechambua jamii katika muktadha wa ndoa na familia. Anasema kwamba mara nyingi maisha katika ndoa hupata msukosuko na kutetereshwa na kujilimbikizia mali kwa wachache, hali ambayo inatokana na ubinafsi.

Ubinafsi na kiburi ni miongoni mwa visababishi vikuu vya mgogoro wa ndoa. Watu wengi huathiriwa na tabia hizi. Watu walio na ubinafsi na kiburi hupungukiwa na sehemu fulani ya akili ambapo hukubali tabia zao tu na kukataa za wengine na hawataki kukubali makosa yao. Ni hatari sana ambapo ghasia ya tabia inafanikishwa na mtu mwingine yaani, kuwakosoa wengine kwa makosa yao. Wakati mwingine mume na mke wote husumbuliwa na tatizo hili kwa maana hiyo, watagombana kila siku. Kila mmoja atamlaumu mwenzake na wakati huo huo kila mmoja wao atakataa kuhusika kabisa na makosa yote.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* Majununi na Michelle walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Mwanzoni, Majununi alikuwa akiishi hemani. Akamwalika Michelle kwenda kumtembelea. Majununi alipoenda kumlaki kutoka kwa helikopta, Michelle alikataa kushuka. Michelle alimwambia Majununi, "Monsieur Major Noon, nasikitika sana sitakanyaga chini wayo wa mguu wangu. Jenga nyumba, acha ujuba. Siwezi kuishi hemani humu mwituni kama maskini sina sinani nikiulizwa siungami." Majununi alijenga nyumba ya matofali yenye vyumba vinne lakini Michelle akaita kibanda. Majununi akajengesha kasri ambalo nalo Michelle hakufurahishwa nalo kwa idadi ya vyumba. Kwa sababu ya kiburi na ubinafsi, uhusiano wao ulikatika.

Kuna mgogoro kati ya Mtemi Nasaba Bora na bibiye Zuhura. Zuhura anamshauri Mtemi Nasaba Bora ili kumsaidia awe mtawala wa kujali maslahi ya watu wake. Mfano anamtahadharisha Mtemi kuhusu Amani na Imani kuwa hawana makosa. Pia anamshauri ampeleke kijana DJ hospitalini baada ya kungatwa na mbwa wao lakini Mtemi Nasaba Bora anamjibu kwa kiburi na kuonyesha kutojali.

Kuna mgogoro kati ya Dora na Mwalimu Majisifu kwa sababu ya ubinafsi na kiburi. Mwalimu Majisifu hakujishughulisha kumsaidia mkewe kufanya kazi za nyumbani; alimwachia zote huku yeye akijistarehesha tu. Mwalimu Majisifu anajisifu kuwa "hakuna mwandishi bora kuliko mimi Shakespear wa Afrika… a writer of distinction" (uk. 44). Majisifu anadharau na kumtusi Dora kwa sababu yeye ni msomi. Dora naye kwa sababu anamwelewa mumewe, na kuwa ni mwizi wa miswada, anamkejeli Majisifu kuwa hawezi kuandika chochote, "kwani waweza kuandika nini?" (uk. 44). Majisifu anajiona bora kuliko mkewe Dora na hataki kujibizana naye "Shut up! …unadhani kujipaka hizo wanja kunakufanya uwe sawa na mimi?" (uk. 45).

## Mawasiliano Finyu

Mawasiliano ni muhimu katika jamii kwa sababu yanahimili ushirikiano na hali kadhalika kuboresha uhusiano wa maendeleo. Wataalamu wa masuala ya ndoa Burleson na Denten (1997, uk. 84) [4] wanasema kuwa mawasiliano ni wajibu muhimu katika ndoa. Ni jukumu la kila mwanandoa kuwasiliana vyema na mwenzake. Baadhi ya ndoa zilizomo katika riwaya teule za utafiti wetu zinakumbwa na changamoto za ukosefu wa mawasiliano bora kwa hivyo kusababisha kuvurugika au kuwa na migogoro katika ndoa.

Mawasiliano yanapovunjika katika mahusiano, ugomvi ni jambo la kawaida kutokea. Ogechi (2002, uk. 7) [20] anasema kuwa ili mawasiliano yafanikiwe lazima pande zote mbili ziwe tayari kuwasiliana. Iwapo mapenzi watashindwa kuelezana hisia zao, mawazo yao, mitazamo yao, imani zao, matatizo yao au hata furaha zao, uhusiano utakuwa unaelekea pabaya. Kama wanandoa hawazungumzii matatizo na vikwazo wanavyokutana navyo katika mahusiano yao na kuviondoa kunazuka migogoro. Wengine hawana lugha nzuri za mawasiliano. Hawajui wakati gani waseme nini na wakati gani wasiseme. Shida nyingine inatokea wakati mmoja wa wanandoa au wote wawili kutotaka kumsikiliza mwenzake. Mawazo yake iwe ya vitu au ya kimwili kwa ukaidi au kutokuwa na uwezo wa kutimiza au kutokuwa tayari kumsikiliza mwenza mantiki yake katika hitaji husika.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, kuna ukosefu wa mawasiliano bora kati ya Mtemi Nasaba Bora na bibi yake Zuhura. Zuhura anamshauri Mtemi Nasaba Bora ili amsaidie awe mtawala mwenye kujali maslahi ya watu wake lakini mawasiliano hayo yanasababisha ugomvi. Mfano, Zuhura anaposisitiza kuwa DJ apelekwe kwa matibabu, ugomvi unazuka baina yake na Mtemi Nasaba Bora. Aghalabu, Mtemi Nasaba Bora hakutaka mkewe azungumze naye hasa akiwa anamrekebisha kitabia. Zuhura anapomweleza Mtemi Nasaba Bora kuwa anastahili kuwa mfano mzuri kwa wana wake, Mtemi Nasaba Bora anamjibu kwa ukali. "Shut up! Acha kuzungumza kama mwanamke mpumbavu!" (uk. 105).

Kuna mgogoro wa familia baina ya Mwalimu Majisifu na mkewe Dora. Mgogoro haukuwa jambo geni kwao bali ndivyo yalivyokuwa maisha yao ya kila siku. Hakukuwa na mawasiliano mazuri kati yao. Wawili hawa wanazungumziana kwa kelele na wanaishia kutupiana cheche za matusi.

## Watoto

Watoto katika jamii zote za kiafrika huendeleza kizazi. Njue na Rombo (2007) [17] wanaeleza kwamba katika jamii za Kiafrika ni lazima mtu aliyekomaa aoe na kupata watoto ili atambulike kwamba amekamilika. Wanaeleza kuwa watoto wa kiume wanapendelewa zaidi ya wale wa kike. Suala la watoto husababisha changamoto katika ndoa. Kuna wale wanakosa kuzaa watoto na jambo hili husababisha ugomvi kati ya mume na mke na aghalabu lawama kumwendea mwanamke. Wengine huzaa watoto walemavu na kusababisha huzuni katika ndoa kila mmoja akimlaumu mwingine na kusababisha unyanyapaa kwa watoto walemavu. Watoto wanapozaliwa, mara nyingi huja na changamoto zao. Watoto hawa wanaweza kupunguza mapenzi baina ya mke na mume hasa wakiwa wachanga au ndio wanakuakua. Kunakuwa na mgogoro wa kindoa kuhusu ufundishaji wa nidhamu kwa watoto, kurudi watoto, chakula na malezi ya watoto. Watoto wengine huiga tabia potovu za wazazi wao na kusababisha huzuni katika familia.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, kuna mgogoro kati ya Mwalimu Majisifu na mkewe Dora kwa sababu ya watoto wao. Mkewe Mwalimu Majisifu anapojifungua watoto pacha ambao hawana uwezo wa kutembea, mumewe anataka kuwatupa majini lakini mkewe anamsihi asifanye hivyo. Dora anamwambia Majisifu, "Mtoto ni mtoto hata likiwa bonge la nyama" (uk. 31). Majisifu alimlaumu Dora kuwa yeye ndiye kisababishi cha wao kuzaa watoto walemavu. "Lazima mwanamke huyu kafanya madhambi huko kwao alikotokea ndiyo maana kanizalia mashata haya ya binadamu. Mwanamke mjalaana

asiyejua kuzaa wana ila hunipokelea masimbi na mashata tu." (uk. 31).

**Kutowajibika**

Kutowajibika ipasavyo huchangia pakubwa kuwapo kwa migogoro kwenye familia. Mizozo hutokea iwapo mume au mke hawajibiki kwa kutenda impasavyo kama mume au mke au kusaidiana kufanya shughuli fulani. Mfano, imekuwa kama utamaduni kwa waafrika kuacha kazi nyingi kama si zote za nyumbani kwa mke. Kama mume mwenyewe hajishughulishi na kufanya baadhi ya kazi za nyumbani au kuajiri mfanyakazi, ni wazi kutakuwa na ugomvi. Haya hutokea pale mume hurandaranda tu bila kujali maslahi ya watoto na mke wake na kurudi nyumbani akiwa amelewa chakari na kutaka kuhudumiwa. Katika ulimwengu wa sasa wanawake na wanaume wote huondoka kutafuta riziki. Bila kuwa na mgawanyo mzuri wa kazi nyumbani mmoja huweza kulemewa na zaidi kuzusha migogoro mingine.

Kutojali na kutokuwa na msaada kwa familia ni jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linaumiza sana na kusababisha kushuka kwa thamani ya mapenzi miongoni mwa mahusiano mengi. Wengine wanatoroka majukumu yao na kukataa kuwajibika. Maisha ya wapenzi wengi yamekuwa yakipoteza maana kiasi cha kufikia kuchuja kutokana na wapenzi wenyewe kuwa na mawazo ya ubinafsi. Utakuta watu wameoana lakini kila mmoja anakabili changamoto za maisha peke yake, hali ambayo humfanya atumie nguvu kubwa kutafuta ushindi wa matatizo yake. Kutowajibika ipasavyo huchangia pakubwa kuwapo kwa migogoro kwenye familia zisizohesabika. Mizozo hutokea iwapo mume hawi kiongozi. Ni lazima awajibike.

Erapu (1977) [10] anaeleza kuwa katika ndoa yoyote, mume na mke wana jukumu la kuhakikisha kuwa uhusiano wao umeimarika na kudumu. Wakati mmoja anahisi kwamba majukumu yote ya familia yanastahili kutekelezwa na mwenzake pekee, kunakuwa na mianya ambayo inasababisha migogoro ya ndoa.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* mgogoro unatokea kati ya Dora na Majisifu, Zuhura na Mtemi Nasaba Bora kwa sababu ya kutowajibika. Dora anamlalamikia mumewe Mwalimu Majisifu kuwa tangu Imani aende kwa nduguye, kazi imemlemea huku Majisifu akilaza damu tu na kuchapa mtindi.

We, bwana unafikiri n'natumia petrol nini? Hii siku ya tatu tangu Imani ende kwa nduguye na bado hajaonekana. Wewe ndiye ulo'mpa ruhusa ya kwenda. Sasa kazi zimenilemea na kunisonga. Mwenyewe unalaza damu tu, hupiki hupakui. Unachojua ni kuchapa mtindi tu. Haya ni maisha gani haya? (uk. 44).

Mwalimu Majisifu hakujishughulisha kumsaidia mkewe kufanya kazi za nyumbani, alimwachia zote huku yeye akijistarehesha tu.

Mgogoro unazuka kati ya Zuhura na Mtemi Nasaba Bora. Mtemi Nasaba Bora kila mara anaondoka kusulihisha mgogoro wa shamba. Zuhura ndiye anatakikana kufanya kazi za nyumbani kama kushughulikia wanaotafuta kazi pale nyumbani na shughuli za nyumbani kama kukama ng'ombe. Kazi inapomlemea Zuhura anamlalamikia Mtemi Nasaba Bora kwa kuwafunga vijana Imani na Amani bila hatia na pia Amani alikuwa anawasaidia kazi nyumbani. "Ngo'mbe wanaumia mno. Sasa ngo'mbe hawakamwi, hawanyeshwi maji. Amani kafanya kazi hapa vizuri kwa miaka miwili" (uk. 105).

**Kushikilia Mila na Desturi zilizopitwa na Wakati**

Utamaduni hubadilika jinsi nyakati zinavyoathiriwa na mabadiliko ya kiteknolojia na utandawazi. Jamii za riwaya za utafiti zinakumbwa na changamoto za kuzingatia mila na desturi zao za jadi pamoja na kuwepo haja ya kufumbata usasa. Changamoto hizi ni athari hasi katika baadhi ya ndoa zilizoko katika riwaya teule za utafiti. Katika jamii hasa za kiafrika, kuna imani potofu mbalimbali kuhusiana na wanawake na wanaume.Kuna imani potofu kuhusu utaratibu wa kazi. Wanaume wengine hawataki wanawake kufanya kazi na wanawaambia waache kazi na kukaa nyumbani au kuwashuku wakiwa kazini au wakichelewa kurudi nyumbani mapema.

Kila mwanajamii hutamani kuheshimiwa, kusikilizwa na kupewa haki yake. Hata hivyo jamii nyingi za kiafrika humtarajia mwanamke kumheshimu mume na kumnyenyekea. Wanawake wengi huelekezwa na matakwa ya waume wao jambo ambalo linazua ugomvi au kutoelewana katika ndoa. Wakielezea hali yenyewe, Nunes na Dearma (1976, uk. 96) [18] wanaelezea kuwa ndoa inamtosa mwanamke katika hali chukivu ya kuwa mtumishi wa mumewe na katika kutaka kujikwamua kutoka hali hiyo, mgogoro unazuka kati ya mume na mke. Hali hii inadhihirishwa na waandishi wa riwaya zetu za utafiti.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, kuna imani potofu kuwa kazi zote za nyumbani hutekelezwa na wanawake hivyo wanaume kulaza damu na kuwachia wanawake majukumu yote. Dora ametwikwa jukumu la kuwalea na kuwalinda watoto wake ambao wote ni walemavu. Licha ya kuwa Mwalimu Majisifu amesoma hadi chuo kikuu, anashikilia utamaduni wa kale uliopitwa na wakati. Kwa mfano, anamlaumu mke wake Dora kwa kuzaa watoto walemavu. Pia anaona kuwa mwanamke anafaa kunyamaza mbele ya mwanamume na kuwa hapaswi kujibizana naye. Dora anapobishana naye kuhusu umahiri wake katika uandishi anasema, "Nilioa mke au mume mwenzangu jamani?" (uk. 51). Kwingineko Majisifu anamuuliza Dora, "Unanijibu mimi kaa…ma kama mwanamume?" (uk. 45). Imani hii potofu kuhusu wanawake na wanaume inasababisha mgogoro kati ya Mwalimu Majisifu na mkewe Dora.

Ndoa ya Mtemi Nasaba Bora na Bi. Zuhura ilijawa na migogoro ya mara kwa mara. Mtemi Nasaba Bora aliamua kumtaliki mkewe Zuhura kutokana na tuhuma kwamba alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Amani ilhali yeye mwenyewe alikuwa mzinifu na hata kuzaa mtoto na Lowela bintiye Maozi. Katika jamii, mwanamke anatarajiwa kuwa mwaminifu lakini mwanamume ana haki ya kufanya anavyotaka.

**Mmoja Kumdhibiti mwenzake**

Inapotokea kuwa mmoja wa wapenzi anataka kumdhibiti mwenzake na kumwendesha mithili ya mtu anayemwendesha farasi, uhusiano unaohusika utakosa mapenzi na hiyo itakuwa sababu kubwa ya kuzozana kwa wapenzi hawa hata kuachana baadaye. Mtu anaweza kumbana mwenzake kwa kumfuatilia muda wote, kumtishia. Mathalani anapochelewa nyumbani au kwenye miadi na kutompa ruhusa na uhuru wa kupanga ratiba zake, kutangamana na watu wa karibu naye, kutoa uamuzi wowote kuhusu chakula, mavazi, fedha miongoni mwa mengine.

Inapotokea kuwa mmoja tu ndiye anayetoa maamuzi

kuhusiana na shughuli mbalimbali, uchaguzi wa marafiki, maswala ya kifedha, maswala ya nyumbani na mengineyo, mwingine anaweza kujiona kama vile hana nafasi katika ushirika huu, hivyo kuamua kujitoa. Iwapo itatokea mmoja wa wanandoa au wapenzi akijisi kuwa ametengwa katika maamuzi ya msingi yakiwamo yale yanayohusiana na mustakabali wa maisha yake, ni rahisi mgogoro kuzuka.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* Mtemi Nasaba Bora alitia hofu kwa mkewe Zuhura ili kumdhibiti. Alimtia Zuhura uoga ili asimdadisi na pia kuuficha uovu wake. Kwa mfano hakutaka mkewe amdadisi kuhusu kwenda kwake nyumbani akiwa amechelewa na uzinifu wake. Mwandishi anaeleza,

kama ilivyo ada yake usiku uliotangulia alikuwa kenda kwa shughuli fulani alizoziita kusuluhisha 'mgogoro wa ardhi'. Bi Zuhura hakudadisi zaidi. Udhuru wa mumewe wa cheleo la kila siku ulikuwa wimbo uliozoelewa. Bi Zuhura alituhumu kuwa huo 'mgogoro wa ardhi' ulikuwa na kocho ya maana. Pengine kulikuwa na mengi zaidi ya maneno hayo matatu. Lakini afanyaje tu? Mtemi Nasaba Bora alikuwa mume mkali asiyesemezeka wala kuambilika hasa na mwanamke mnyonge kama yeye (uk. 90).

**Tofauti za Asili ya Wanandoa**

Kila mwanadamu ana asili yake ambayo ni tofauti na mwingine. Mwanandoa anaweza kuwa na tabia ambazo zinakera, zinakasirisha na kumsumbua mwenzake na hataki au hajaribu kuzibadilisha au kushauriwa kuhusu tabia hizo. Haichukui muda mrefu kwa wenza wa ndoa kung'amua kwamba hawafaani kama walivyodhani wakati wa uchumba. Maisha ya ndoa hufunua tabia zilizofichika wenzi hao walipokuwa waseja. Watu wengi huingia katika maisha ya ndoa wakiwa na tofauti kubwa sana katika mtindo, tabia na mielekeo. Wenzi wengi wa ndoa hawajui namna ya kutatua tofauti hizo hivyo kusababibsha migogoro katika ndoa. Uchoyo, uchafu, hasira na uropokaji ni mifano ya asili ya binadamu. Wanandoa wengine wamewafukuza wenzao nyumbani kwa sababu ya ukali na kusema matusi. Wanandoa wengine pia wameshikwa na hofu kuhusu matusi, na mapigo ya wenzao. Asili zingine kama ulevi hupelekea mtu kutoelewana na wenzake. Kutowajibika, kukosa heshima na kuonekana mjinga katika jamii husababisha migogoro.

Katika *Kidagaa Kimemwozea***,** tabia ya ulevi na upyaro zinasababisha mgogoro kati ya Dora na Mwalimu Majisifu. Mwalimu Majisifu anatumia muda wake mwingi akipiga mtindi. Bibiye Dora analalamika kuwa mumewe amemwachia kazi yote ya kuwatunza watoto wao walemavu huku yeye akishinda ulevini. Mwalimu Majisifu anawachukia sana watoto wake walemavu na kuwaona kama mashata na masimbi. Pia anamchukia mke wake Dora kwa kumzalia watoto wale ambao kwake si binadamu. Chuki hii inamfanya kuzama kabisa katika ulevi kama njia ya kujisahaulisha matatizo yake.

Katika mafarakano yake, Mwalimu Majisifu na Dora, alizoea kumtusi na kumwita majina mengi ya kumdunisha. Kwa mfano anamwambia, "Bloody Bastard….Bwege wee….Domo kaya wee...!" (uk. 44-45). Dora alikeketeka maini kutokana na maisha ya ulevi na matusi ya mumewe Mwalimu Majisifu. Mwandishi anaeleza, "Mambo yalikuwa mabaya zaidi Majisifu alipouchapa mtindi kama sasa na kuufanya mdomo wake karakana ya matusi" (uk. 44). Ndoa ya Mwalimu Majisifu na Dora haikuwa na amani. Aghalabu Mwalimu Majisifu alikuwa mlevi kwa hivyo hakuweza kumsaidia mkewe katika kuwalea watoto punguani na viwete. Wakati mwingine Dora akidai haki ya kusaidiwa na mume wake aliishia kutukanwa tu.

Uzinifu wa Mtemi Nasaba Bora na kuchelewa kwake kurudi nyumbani kunamwacha Zuhura katika hali ya upweke na hakuweza kudadisi matendo na mienendo ya Mtemi Nasaba Bora. Pia aliogopa kumwambia mumewe, Nasaba Bora kuhusu upweke wake na kiu yake ya mapenzi kwa sababu Mtemi Nasaba Bora ni mkali. Mwandishi anaeleza, "Lakini afanyaje tu? Mtemi Nasaba Bora alikuwa Mume mkali asiyesemezeka wala kuambilika, hasa na mwanamke mnyonge kama yeye" (uk. 90).

**Wanandoa Kutokuwa Tayari Kuungama Kosa, Kujirekebisha na Kusameheana**

Kisababishi kingine cha mgogoro katika ndoa ni wanandoa kuwa na tabia ya kutoungama makosa na kujirekebisha. Wengine kwa kiburi hurudiarudia makosa. Huenda mwanandoa ameshaambiwa mara nyingi na mwenzake kuhusu tabia yake na pengine habadiliki. Kila siku anarudia makosa yale yale ambayo yanamuumiza mwenzake na kusababisha malalamishi katika ndoa. Si watu wengi ambao wako tayari kusamehe na kusahau makosa. Kosa la awali litakumbushwa tena na tena na kuzidi kuchochea ugomvi hata uliokuwa mdogo na kuonekana mkubwa kwa sababu tu umehusishwa na makosa yaliyopita. Wengine hawako tayari kuombana msamaha bila kujali nani mwenye kosa.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* ndoa kati ya Mwalimu Majisifu na Dora ilikumbwa na migogoro kila mara kwa sababu ya wanandoa hawa kutokubali makosa yao na kusameheana. Dora anajuta siku ambayo alifunga pingu za maisha na Mwalimu Majisifu. Ndoa yake na mumewe haijamfurahisha na imempa majuto katika maisha yake. Mwalimu Majisifu anamlaumu mkewe peke yake ilhali watoto ni wao wote na ni wote waliochangia kuwapata. Mwalimu Majisifu badala ya kukubali upungufu wa watoto wao na kushirikiana kuwapenda anazua ugomvi kwa kumlaumu mkewe.

Mwalimu Majisifu anajisifu kuwa, "Hakuna mwandishi bora kuliko mimi. Shakespear wa Afrika. yuko wapi? Am a writer of distinction" (uk. 44). Mwalimu Majisifu anadang'anya kuwa yeye ndiye aliyeandika *Kidagaa Kimemwozea.* Anapata sifa za bure Tomoko na hata Afrika. Dora alitilia shaka uwezo wa mumewe wa kutoa hotuba katika chuo kikuu. Hii ni kwa maana alijua fika kuwa siye mumewe aliyeandika riwaya hiyo maarufu. Dora anamwambia Mwalimu Majisifu hivi, "kama utaweza, mbwa apige mswaki" (uk. 51). Maoni haya ya Dora yalichochea zaidi mgogoro baina yao. Mwalimu Majisifu hataki kuomba msamaha kwa wizi wake wa miswada na Dora hayuko tayari kumsamehe na kumwelewa.

Mtemi Nasaba Bora anampa talaka mkewe ambaye alikuwa mwaminifu kwake kwa tuhuma za kuwa na jicho la nje na Amani. Hata ingawa Mtemi Nasaba Bora mwenyewe anazini haoni kuwa mkewe anastahili kutimiziwa haja zake za kimapenzi. Talaka hii inatokana na wazo kuwa mkewe Mtemi Nasaba Bora alipatikana na Amani katika chumba chake cha kulala usiku wa manane na hivyo Mtemi Nasaba Bora akajiamulia kwamba mkewe alimwendea kinyume. Anayafanya haya na yeye mwenyewe ana mpenzi wa pembeni ambaye ni Lowela Maozi. Mtemi Nasaba Bora hataki kusikiliza maoni ya mkewe wala kujirekebisha kutokana na tabia yake ya uzinifu.

**Dharau**

Dharau katika ndoa hupunguza mapenzi na kusababisha

migogoro. Dharau mara nyingi hutokea pale mmojawapo wa wanandoa akimzidi mwenzake uwezo iwe kwa cheo, pesa, elimu, uzuri au hata akili.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, uhusiano kati ya Michelle na Majununi ulikoma kwa sababu ya Michelle kumdharau na kumkataa Majununi. Michelle, msichana Mfaransa alimfanya Majununi kulijenga jumba la kifahari kwani Michelle alidai kuwa angeolewa kwake tu iwapo Majununi angejenga jumba kubwa kulingana na daraja lao. Hata hivyo Michelle hakuolewa na Majununi. Michelle alimwambia Majununi kuwa hawangeweza kuoana kwa sababu hawakufaana kwa vyovyote vile. "Monsiuer Major Noon," alisema Michelle hatimaye, "Niwie radhi sana lakini naona hatufaani" (uk. 17-18).

Mwalimu Majisifu anamdharau na kumdunisha mkewe Dora. Anamwona Dora kama kiumbe anayestahili kufanya kazi zote za nyumbani. Mwalimu Majisifu hamsaidii mke wake kufanya kazi yoyote ya nyumbani. Analaza damu tu na kuchapa mtindi. Mwandishi anasema, "Dora alisimama sebuleni na kumwangalia mumewe aliyekuwa kajinyoosha kochini kalewa chopi. Haya ni maisha gani? Alikeketeka maini Dora" (uk. 44). Aidha Majisifu anamtusi mkewe kila uchao. Mwalimu Majisifu alimwonea Dora na alijiona bora kuliko yeye. Mwalimu Majisifu analaumu mkewe kwa kuwazaa watoto walemavu.

Mwalimu Majisifu anamtoa Amani kwenye zahanati, anampeleka kwake bila kumshauri wala kumridhia Dora. Majisifu alijiamulia peke yake. Mwandishi anasema,

Walipofika nyumbani kwa Mwalimu Majisifu Dora alifoka kwa Hasira... mbona Majisifu kujiamulia peke yake kuleta mgonjwa hapo kwao? Mbona? Hajui kwamba tayari maskini Dora alikuwa kalemewa na mzigo wa wale watoto wawili waliokuwa wamelemaa akili aliokuwa akiwatunza (uk. 138-139).

Hiki kitendo kinaoonyesha kuwa Mwalimu Majisifu hakuchukulia mkewe kuwa sawa naye na kwa hivyo hakumthamini, jambo ambalo lilizua mgogoro kati yao. Dora naye anamdharau mumewe kwa kuelewa kuwa yeye si mwandishi vile alivyokuwa akijulikana na kwamba asingeweza kutoa mhadhara katika chuo kikuu cha Mkokotoni. Majibizano makali yanazuka kati yake na Majisifu. Dora anamwambia Majisifu, "Kwani waweza kuandika nini?... Sijawahi kumwona kibogoyo akiguguna mfupa. Siku moja isiyokuwa na jina siri zake zitafichuka na hila zako zikutokee puani" (uk. 44).

Mtemi Nasaba Bora harejei nyumbani kwa wakati uliofaa. Yeye huja nyumbani usiku wa manane au jogoo la kwanza. Anapokuja anamwamsha mkewe kila mara mkewe hukosa usingizi kutokana na kuchelewa huku. Hii ni njia mojawapo ya kutomthamini bibiye kutokana na taasubi ya kiume. Mwandishi anasema kuwa, "Kwake Bi. Zuhura wanaume wangewastahi wanawake kidogo, wawaone kama abiria wenzao katika mashua ya maisha, dunia ingekuwa pahala pema pa kuishi" (uk. 91). Hii ni ithibati tosha kuwa katika jamii hii, wanaume wamejiona bora kuliko wanawake na hawawachukulii kuwa binadamu walio sawa nao.

**Tamaa Iliyokithiri**

Tamaa ni kitu kingine ambacho hufanya mahusiano mengi kukosa nguvu na mengine kuvurugika kabisa. Kunakuwa na tamaa mbalimbali ambazo huvuruga ndoa kama tamaa ya pesa, vyeo, uongozi kwa njia isiyo halali. Hali ya kutamani maisha makubwa ambayo ni nje ya uwezo husababisha ugomvi. Lungo (1981, uk. 42) [13] katika shairi la *'Tamaa'* anasema kuwa tamaa inaweza kumfanya mtu kuwa hayawani na kutenda yasiyofaa. Naye Engels (1985) [9] anasema kuwa ndoa na familia nyingi huvunjika kwa sababu kilichoziunganisha awali ni ubinafsi wa tama ya mali wala sio udhati wa mapenzi. Mwelekeo huu unaonyesha kuwa iwapo wahusika katika ndoa na familia wangekuwa na usawa wa kumiliki mali, ubinafsi ungefifishwa na hivyo kukuza ushikamano katika jamii.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, kuna migogoro ya ndoa kwa sababu ya tamaa mbalimbali miongoni mwa wanandoa. Majununi na Michelle walikuwa na uhusiano wa kimapenzi. Majununi alikuwa na tamaa ya mapenzi. Alimpenda sana Michelle. Michelle vile vile anamtamani sana Majununi lakini ndoa yao haikuwezekana kwa sababu Michelle alikuwa na tamaa ya nyumba nzuri. Majununi naye akashindwa kumjengea nyumba kama hiyo. Kwa sababu ya tamaa ya mali, starehe na anasa, Michelle alimkataa Majununi jambo ambalo lilisababisha Majununi kuamua kutooa maishani mwake mwote.

Mtemi Nasaba Bora alikuwa na tamaa ya mapenzi. Aliweza kuwatamani wanawake wengine japo alikuwa ameoa. Alikuwa anamwacha mkewe nyumbani na kwenda kushiriki mapenzi na wanawake wengine kama vile Lowela Maozi. Aliweza hata kumdunga msichana huyu mimba. Tabia yake hii ilimfanya mkewe Bi. Zuhura kubaki mpweke na kuandamwa na tamaa kubwa ya mapenzi. Hata akawa anahusudu wanawake waliokuwa hawaachiwi upweke na waume zao japo ni maskini.

Mwalimu Majisifu alikuwa na tamaa kubwa ya pombe. Kwake pombe ndio ilikuwa ibada (uk. 93). Kulewa kwake kulimfanya kutowajibika kusaidia kulea watoto wao walemavu, jambo ambalo lilizusha mgogoro kati yake na Dora kila mara. Dora alijuta kuolewa na Mwalimu Majisifu.

**Kutovumiliana Katika Maisha ya Ndoa**

Mume na mke, kama wanadamu, kila mmoja ana kasoro zake. Hivyo ni jambo la kawaida kwa mume au mke kumkosea mwenzi wake. Pakikosekana kuvumiliana na kusameheana, ndoa huwa mashakani. Mara nyingi vijana walio wengi wamejiingiza kwenye mapenzi bila kufahamiana vizuri na wenzi wao au bila hata kuwa na maandalizi ya kutosha ya kuwa na familia. Matokeo yake ni ndoa kuvunjika.

Katika *Kidagaa Kimemwozea,* Mtemi Nasaba Bora ni mhusika ambaye hawezi kuwavumilia wengine. Mtemi Nasaba Bora alipowapata mkewe Zuhura na Amani chumbani mwao, aliwashuku kuwa na uhusiano wa kimapenzi, tuhuma ambazo hazikuwa na mashiko. Mtemi hakumpa mkewe wala Amani nafasi ya kujitetea. Alifanya maamuzi ya kumpa talaka mkewe Zuhura, jambo ambalo halingetokea kungekuwa na kuvumiliana na kuelewana kwa pande zote za Mtemi Nasaba Bora na bibiye Zuhura. Mtemi Nasaba Bora alimtuhumu Zuhura kutokuwa mwaminifu katika ndoa, jambo ambalo halina mashiko ilhali yeye ni mkware na Zuhura anajua na kuvumilia. Mtemi Nasaba Bora alimpa Lowela ujauzito na kuzaa naye kitoto Uhuru. Kila wakati alitoa udhuru wa kwenda kusuluhisha migogoro ya ardhi na kwenda kwa wapenzi wake wa pembeni. Bibiye alimtuhumu lakini hakuweza kumuuliza mumewe kilichokuwa kikiendelea (uk. 39).

Ndoa kati ya Dora na Mwalimu Majisifu ilikumbwa na mgogoro wa mara kwa mara kwa sababu ya kutovumiliana. Ndoa yao ilikumbwa na kelele na kutupiana cheche cha

matusi. Hawa wawili walishinda wakizozana bila kutaka kuelewana. Mwandishi anaeleza, “Dora alijutia siku aliyokubali kufunga pingu za maisha na Mwalimu Majisifu” (uk. 44).

**Migogoro Binafsi**

Wanandoa wengine huruhusu migogoro yao binafsi, iwe ya kazini au wapi ambayo haina mahusiano na ndoa zao kuharibu ndoa zao.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, Mtemi Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu wana mgogoro wa kinafsia ambao unahamishwa kwa familia na kusababisha kutoelewana. Mtemi Nasaba Bora anaongea na mkewe kwa kelele na kutomruhusu kuongea. Mkewe Zuhura, alikuwa anamkosoa na kumshauri aache kutawala watu kidekteta lakini Mtemi Nasaba Bora hataki kuongea naye. Mtemi Nasaba Bora, anapopata barua kutoka kwa Lowela Maozi, mpenziye wa pembeni kumjulisha awaachilia Amani na Imani la sivyo atoboe siri kuhusu uhusiano wao wa kimapenzi, anaongea na mkewe Zuhura kwa ukali na kumtusi. Anapowapata Amani na Bi. Zuhura katika chumba cha kulala anawashuku kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Akamtusi Zuhura na kumpa talaka.

Mgogoro wa nafsia wa Mwalimu Majisifu kuhusu watoto wao walemavu unasababisha kutoelewana kati yake na mkewe Dora. Alifikiri kuwa chanzo chake ni laana za upande wa Dora. Watoto walemavu wa Mwalimu Majisifu hawakufahamu lolote.

Hili ndilo lililomsononesha Mwalimu Majisifu. Kwani nini yeye tu ndiye aliyetupiwa watoto waliokuwa hasa kiporo cha uumbaji? Kwani yeye alikosa kosa gani ambalo halina msamaha hata astahili adhabu kadri ile?... Akamchukia mkewe pia kwa kumzalia masimbi hayo. Lazima mwanamke huyu kafanya madhambi huko kwao alikotokea ndiyo maana kanizalia mashata haya ya binadamu. Waama, watu wachache sana walipata kujua kwamba Mwalimu Majisifu aliwalilia ngoa wazazi wengine. Aliwaonea gere kwa kupata kile ambacho yeye hakupata (uk. 30-31).

**Ukatili na Dhuluma**

Azimio la Umoja wa Mataifa (1993) juu ya kumalizwa kwa dhuluma dhidi ya wanawake linatafsiri dhuluma kama kitendo chochote ambacho huleta madhara au kinaweza kuleta madhara ya kimwili, kimapenzi au kisaikolojia pamoja na vitisho vya vitendo hivi na kufanya jambo au mambo pasi na hiari. Chapman (2008, uk. 121-166) [5] ameeleza jinsi dhuluma zilivyo katika ndoa. Anaeleza kuwa mamilioni ya wanawake na wanaume huathirika kila mwaka kutokana na ukatili na dhuluma katika ndoa. Kuna aina mbalimbali za dhuluma ambazo hujitokeza baina ya wanandoa na si lazima kwamba mwanamume ndiye anayenyanyasa mwanamke.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, ukatili baina ya na kwa wanandoa kunasababisha kutoelewana. Mwalimu Majisifu anamlaumu mkewe kumzalia watoto walemavu. Alitaka kuwatupa wanawe majini walipozaliwa bila miguu lakini Dora akamzuia kwa bembelezi laini, “Mtoto ni mtoto hata likiwa bonge la nyama” (uk. 31).

Mtemi Nasaba Bora alimdhulumu mkewe Zuhura kimapenzi. Ndoa yao haikuwa na furaha. Ilikuwa na matatizo hapa na pale. Mtemi hakuwa na wakati wa kumridhisha mkewe kimapenzi. Kila mara alijidai alikuwa anakwenda kusuluhisha ‘migogoro ya shamba’. Wakati huo huo Mtemi alikuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa na kumwacha Zuhura katika upweke. Mwamdishi anaeleza, “Bi. Zuhura alijiona maskini wa mapenzi katikati ya mali isiyodhihirika” (uk. 90). Bi. Zuhura alifungiwa nyumbani akabaki na tamaa ya mapenzi. Mumewe akawa anaenda zake kujifurahisha na wanawake wengine kama Lowela.

**Hila na Udanganyifu**

Baadhi ya wanandoa wanatumia hila na udanganyifu ili kutimiza haja zao. Hii ni changamoto kwa asasi ya ndoa kwa kuwa athari zake ni hasi na aghalabu ni kisababishi cha migogoro katika ndoa nyingi.

Mwanamke katika ndoa ni mtu aliyekaliwa na kutawaliwa kila njia na kwa kutumia kila hila hivi kwamba hana uhuru wowote wa kujiamulia na kutenda mambo yanayomfaidi kama binadamu. Maksuudi alimwoa Mwanasururu kwa lengo la kumunyang’anya mali yake aliyorithishwa na babake. Maksuudi alimhini Mwanasururu haki yake ya uridhi na kumpa talaka bila kujali matokeo yake. Maksuudi alimtawisha Tamima na kukataza mtu yeyote kuingia nyumbani mwao bila idhini yake eti kama njia ya kuikinga na kuinusuru familia yake na ulimwengu mwovu. Hii ilikuwa hila ya kuwazuia Bi. Tamima na Mwanasururu kujua udanganyifu wake wa kudai kuwa alikuwa anaenda kusali katika kaburi la shehe wake ilhali alikuwa anaenda kustarehe na hawara wake Kazija, jambo ambalo baadaye lilisababisha ugomvi baina yao. Mwandishi amewsilisha kwa uwazi na kwa njia ya uhalisi hali halisi ya maisha wa wanandoa.

Katika *Kidagaa Kimemwozea*, hila na udanganyifu wake Mtemi Nasaba Bora kunazusha kutoelewana kati yake na mkewe Zuhura. Mtemi Nasaba Bora anamdanganya mkewe kuwa anaenda kusuluhisha ‘migogoro ya ardhi’ ilhali alikuwa anaenda kushiriki mapenzi na wanawake wengine kama Lowela Maozi. Aidha kulingana na Mzee Matuko Weye, aliwanyang’anya wanaume wake zao (uk. 71). Alipokuwa anafanya hivyo alikuwa anamwachia mkewe upweke mkubwa. Bi Zuhura alibakia kuwaonea gere wanawake ambao walikuwa hawabandukani na waume zao.

**Ulevi**

Reis na Ruth (1993) [23] kutokana na uchunguzi wao wanadhihirisha kwamba dawa za kulevya na pombe huchangia pakubwa katika kusababisha migogoro katika ndoa. Katika *Kidagaa Kimemwozea,* Dora aliishi akilalamikia tabia ya Majisifu ya kulewa. Alidai kuwa kazi yake Majisifu ilikuwa ni kulewa na kumwachia kazi yote ya nyumbani. Dora anamwambia Mwalimu Majisifu, “Mwenyewe unalaza damu tu, hupiki hupakui. Unachojua ni kuchapa mtindi tu” (uk. 44). Kulewa na kutowajibika kwa Majisifu kulisababisha majibizano kati yake na mkewe Dora.

**Hitimisho Na Mapendekezo**

Makala hii imefafanua vichocheo mbalimbali vya migogoro vya kindoa kama vinavyosawiriwa katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Ni wazi kuwa migogoro ni jambo la kawaida katika mahusiano ya kimapenzi na kwa hakika haiepukiki isipokuwa wenza kujifunza jinsi ya kukabiliana nayo na kuondoka wakiwa salama. Kuzifahamu sababu kuu za migogoro katika ndoa kutasaidia wanandoa kujipanga na kutengeneza uhusiano wao ili kuuimarisha.

Kwa sababu ya upeo wa utafiti wetu katika kitabu husika, hatukuweza kushughulikia maudhui ya ndoa kwa kina. Tunapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu migogoro katika

ndoa kwa kutumia nadharia ya Uhalisia au nyingineyo katika vitabu vinginevyo vya fasihi ya kiswahili. Sababu ya kupendekeza jambo hili ni kuwa migogoro katika ndoa ni shida jambo ambalo limekuwa dondandugu katika jamii.

**Marejeo**


1. Arege T. *Mwongozo Wa Pango*. Nairobi: Vide Muwa Publishers, 2006.
2. Arege T. *Mwongozo wa Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Target Publications Limited, 2012.
3. Bouchier D. *The Feminist Challenge.* London: Macmillan Press, 1983.
4. Burleson B, Denten W. The Relationship between Communication Skills and Marital Satisfaction: Some Moderating Effects. *Journal of Marriage and Family*, 1997; 59(4).
5. Chapman G. *Desperate Marriage. Moving towards Hope and Healing in Your Relationship*. Chicago: Northfield Publishing, 2008.
6. Collins W, Anderson S. *Collins English Dictionary: Complete and Unabridged*. New York: Harper Collins, 2006.
7. Cutrufelli M. *Women of Africa, Roots of Oppression.* Caledonia Road, London: Zed Press, 1983.
8. Eagleton M. *Feminist Literary Theory.* New York: Basil Blackwell, 1989.
9. Engels F. *The Origin of Family Private Property and the State.* Chicago: Charles H. Ken and Company Co-operation, 1985.
10. Erapu L. *A Student Study Guide of the Burdens.* Nairobi: Heinemann-Educational Books, 1977.
11. Greer G. *The Female Eunuch*. London: Harper Collins Publishers, 1970.
12. Katola E. *Udhalimu dhidi ya Wahusika wa kike katika Tamthilia za Kiswahili* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, 2006.
13. Lungo H. *Malenga ya Mashairi Yetu*. Nairobi: East African Publishing House Ltd, 1981.
14. Maina V. *Nafasi ya Mwanamke Katika Tenzi Mbili za Shaaban Robert; Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili* (Tasnifu ya Uzamili, Haikuchapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, 2005.
15. Maitaria N. *Mwongozo wa Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd, 2012.
16. Mugenda O, Mugenda A. *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press, 1999.
17. Njue R, Rombo D. *Family Strengths and Challenges in Kenya*. New York: The Harwoth Press, 2007.
18. Nunes M, Dearma W. *The Lace Ghetto*. Toronto West: New Press, 1976.
19. Nyaosi K. *Taswira ya Asasi ya Ndoa Katika Riwaya Mbili za Kiswahili: Kiu na Msimu wa Vipepeo* (Tasnifu ya Uzamili, Haikuchapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, 2008.
20. Ogechi N. *Mbinu za Mawasiliano*. Eldoret: Moi University Press, 2002.
21. Ramazonoghlu C. *Feminism and the Contradictions of Oppression.* London: Routledge, 1989.
22. Rao N. *Women and Development.* Punjab: Ashish Publishing House. 1983.
23. Reis T, Ruth W. *Understanding and Preventing Violence*. Washington, D.C.: National Academy Press, 1993.
24. Republic of Kenya *The Matrimonial Causes Ordinance* (chapter 152). Nairobi: Government Printers, 1962.
25. Republic of Kenya *The Constitution of Kenya, 2010: Kenya Gazette Supplement.* Nairobi: The Government Printers, 2010.
26. Sayers J. (Ed.). *Engels Revisited.* London: Tavistoch Publishers, 1987.
27. Walibora K. *Kidagaa Kimemwozea.* Nairobi: Target Publications Ltd, 2012.
28. Wamitila K. *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd, 2002.